

MKATABA WA KUPANGISHA GODOWN

MKATABA HUU umefanyika hapa Arusha leo tarehe 20... mwezi Januari 2024.

KATI YA

GEORGE LAWRENCE MBOYA wa Sanduku la Posta 13633, Arusha (ambaye kwenye mkataba huu ataitwa "Mmiliki") kwa upande mmoja;

NA

SOPHIA GEORGE MBOYA wa Sanduku la Posta 13633, Arusha (ambaye kwenye mkataba huu ataitwa "Mpangaji") kwa upande wapili;

AMBAPO Mkataba huu unashuhudia kama ifuatavyo;

1. Kwamba Mmiliki ndiye mmiliki halali wa eneo lenye Godown lijulikanalo kama kiwanja namba 209, lenye hati namba 38232 na ukubwa wa mita za mraba 1735, lililoko Moshono, Jiji la Arusha, Mkoa wa Arusha.
2. Kwamba Mmiliki amempangishia Mpangaji eneo tajwa hapo juu kwa ajili ya kufanyia biashara.
3. Kwamba mkataba huu ni wa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia tarehe 1 Januari 2024 na kumalizika tarehe 31 Disemba 2028, na baada ya hapo unaweza kurejewa kwa masharti yatakayokubalika na pande zote.
4. Kwamba kodi ya pango ni shilingi laki tatu tu (Tshs. 300,000/=) kwa mwezi ambazo zitalipwa kwa kipindi miezi sita sita; ambapo awamu ya kwanza italipwa wakati wa kusaini mkataba huu na mkataba utaanza tarehe 1 Januari 2024 na awamu zinazofuata zitalipwa kulingana na mkataba.
5. Kwamba Mpangaji amemlipa Mmiliki shilingi milioni moja na laki nane tu (Tshs. 1,800,000/=) wakati wa kuweka saini mkataba huu, ikiwa ni malipo ya pango kwa miezi sita ya mwanzo, ambazo Mmiliki anakiri kuzipokea kwa kuweka saini yake kwenye mkataba huu.

6. Mpangaji atalipa gharama zote za maji, umeme na huduma zote za jamii zitakazotumika kwenye eneo kwa kipindi chote cha mkataba.
7. Mpangaji atazingatia masharti yafuatayo:-
 - (a)Kutunza mazingira kwa usafi na uimara kwa kipindi chote.
 - (b)Kutofanya marekebisho yoyote bila kibali cha mmiliki kwa maandishi.
 - (c)Kutopangisha eneo au sehemu yake kwa mtu mwingine bila ridhaa ya Mmiliki.
8. Kwamba Mmiliki hatambughudhi mpangaji kwa namna yoyote kwa kipindi chote cha mkataba huu, na atawajibika kulipa kodi zote za serikali zinazohusu kiwanja cha biashara.
9. Kwamba endapo upande wowote utataka kusitisha mkataba huu, Upande unaohusika utatoa notisi ya miezi sita kwa upande wa pili, pamoja na fidia ya asilimia mia moja ya kodi iliyolipwa kama ni Mmiliki atakatisha mkataba na kama ni Mpangaji atakatisha hatoruhusiwa kudai kodi yoyote.
10. Kwamba eneo na vitu vyote vitatakiwa kuwa katika hali nzuri na endapo Mpangaji atafanya uharibifu au upotevu wowote atawajibika na matengenezo au manunuzi ya kifaa kilichoharibika.
11. Kwamba Mmiliki atakuwa na haki ya kutembelea eneo husika mara moja kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kupata taarifa ya eneo.
12. Kwamba Mpangaji anaweza kuweka vifaa vyake vingine katika eneo muda wowote wakati wa mkataba huu kama sehemu ya uboreshaji wa biashara yake.
13. Kwamba mkataba huu utavunjika iwapo mpangaji atashindwa kulipa kodi kwa muda wa miezi miwili au zaidi au kwa makubaliano ya pande zote mbili.

UMETHIBITISHWA hapa Arusha tarehe na mwaka uliyotajwa hapa juu.

UMESAINIWA na kutolewa na
GEORGE LAWRENCE MBOYA ambaye
Namfahamu mbele yangu leo tarehe
...²⁰... mwezi Januari, 2024.

.....
MMILIKI

Jina: **FREDRICK ISAYA LUCAS**

Saini

WAKILI



UMESAINIWA na kutolewa na
SOPHIA GEORGE MBOYA ambaye
Namfahamu mbele yangu leo tarehe
...²⁰... mwezi Januari, 2024.

.....
MPANGAJI

Jina: **FREDRICK ISAYA LUCAS**

Saini

WAKILI

